# TUJIFUNZE BIBLIA

*SOMO LA 1*

## BIBLIA IMETOKA KWA MUNGU

Mara nyingi watu wanapoongea kuhusu dini, unaweza kusikia baadhi yao wakisema “Biblia imetoka kwa Wazungu.” Kusudi la somo hili ni kujifunza jinsi tulivyopata Biblia kutoka kwa Mungu na jinsi inavyotubidi kuifuata bila kuongeza wala kupunguza neno. Twafahamu kwamba Biblia imetoka kwa Mungu kwa sababu mbalimbali. Tutaangalia baadhi ya mambo hayo kwa kifupi.

### 1. Jinsi Biblia ilivyoandikwa ni ishara ya kuonyesha kwamba imetoka kwa Mungu.

**BIBLIA** ni neno lililoingizwa katika Kiswahili bila kutafsiriwa. Asili ya neno hili ni neno **biblos** katika lugha ya Kiyunani. Utafsiri wa maneno hayo mawili ni **KITABU**. Ingawa Biblia ni kitabu kimoja, lakini ndani yake vimo **vitabu vidogo 66**. **Vitabu 39** vya kwanza vinaitwa **AGANO LA KALE** kwa sababu vinaeleza habari ya **agano** (au **mapatano**) kati ya Mungu na wanadamu wa kale. **Vitabu 27** vya mwisho vinaitwa **AGANO JPYA** kwa sababu vinaeleza habari ya agano jipya kati ya Mungu na wanadamu wa sasa. Kuandikwa kwa Biblia kulichukua **miaka yapata 1600**. Biblia iliandikwa kwa mikono ya wanadamu walioongozwa na Roho Mtakatifu wa Mungu. Musa alikuwa mtu wa kwanza aliyetumiwa na Mungu; naye aliviandika vitabu vitano vya kwanza. (Vitabu hivyo vinaitwa **TORATI**.) Siku za kale watu hawakuwa na karatasi wala washine ya kuchapa vitabu. La! Bali walikuwa wakitumia mawe, ngozi za wanyama, na mabua ya nyasi badala ya karatasi; na vitabu vyote viliandikwa kimoja kimoja kwa mikono ya watu. Kwa jumla Mungu aliwatumia **wanadamu wapatao 40** katika kuandika Biblia. Watu hawa hawakuishi pamoja ili washirikiane kazi ya kuandika. Waliishi katika nchi mbalimbali na kwa nyakati mbalimbali hata wasijuane. Waliongea kwa lugha mbalimbali nao walitofautiana katika kazi zao. Wengine walikuwa wachungaji, au wafalme, au wavuvi wa samaki, au watoza ushuru, n.k. Wengi wao hawakuelewa hata maana ya maneno waliokuwa wakiyaandika (1 Petro 1:10-12). Kwa hiyo, ilikuwa vigumu wajue kwamba vitabu vyao vitawekwa pamoja visomwe kama kitabu kimoja. Lakini, tunaposoma vitabu vyao hatuwezi kutambua kwamba hawakuelewana wala kushirikiana katika kuandika. **Vyote vinasomeka na kueleweka kana kwamba viliandikwa na mtu mmoja tu! Jambo hili ni ishara kuonyesha Biblia ilitoka kwa Mungu wala si kwa wanadamu!** Mungu aliwatumia wanadamu katika kuiandika Biblia akiwaongoza na Roho Mtakatifu wake. Twasoma, *“Maana unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali **wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu**”* 2 Petro 1:20-21.

### 2. Mafundisho ya Biblia yanaonyesha kwamba imetoka kwa Mungu wala si kwa mwanadamu.

Vitabu vya wanadamu vinaongea mambo ya kimwili. Biblia inaongea mambo ya kiroho ambayo wanadamu wasingaliweza kuelewa kama Mungu asingaliwafahamisha. Kwa mifano: **1)** Wanadamu

wamezoea kuoana na, kwa hiyo, wanafikiri kwamba hata mbinguni wataoana. (Kuna vitabu fulani vya dini ambavyo vinasema kwamba, baada ya kufa kwao wanaume wataingia katika starehe mbinguni na huko wataoa wake wengi watakaowatumikia! Je! Kama vitabu hivi vingaliandikwa na mwanamke wadhani vingaliandikwa hivyo?) Biblia inafundisha kwamba mbinguni watu hawataoana (Luka 20:27-36). Hayo ni mawazo ya kiroho ambayo mwanadamu asingaliweza kujua bila kuambiwa na Mungu. **2)** Wanadamu hudhani kwamba Mungu anao mwili kama sisi. Walakini, Biblia inasema kwamba Yeye ni roho na kwamba roho haina mwili na mifupa (Yohana 4:24 na Luka 24:39). **3)** Wanadamu hupenda kuwasifu wakubwa wao wala hawapendi watu kuandika mambo mabaya kuhusu viongozi wao. Walakini, katika Biblia Mungu ameandika matendo mema na mabaya pia ya watu wa kale. Kwa mfano: Biblia inatueleza makosa ya watu wakubwa kama Ibrahimu (Mwanzo 12:10-20), Musa (Kumbukumbu 32:48-52), Daudi (2 Samweli 11:2-27), Mtume Petro (Wagalatia 2:11-14), na kadhalika. **4)** Walioandika vitabu vya Biblia hawakudai kwamba wameviandika kwa uwezo wao bali walisema waziwazi kwamba waliongozwa na Mungu. Isitoshe, hawakuona haya wala kujaribu kujitetea na kuwashawishi wenzao kwamba kweli ni neno la Mungu, Walisema mara moja tu kwa hakika bila tashwishi. (Watu leo wanaodai kwamba wanaongozwa na Mungu hujitetea sana sana na kuwahimiza watu wawaamini.)

### 3. Biblia inayo mafundisho kuhusu mambo ya sayansi ambayo watu wa kale hawakuweza kuyaelewa.

Watu wa kale waliamini kwamba dunia ilikuwa bapa kama meza. Walidhani kwamba, mtu akitembea zaidi, atafika mwisho wa dunia kisha atatumbukia hewani. Walakini, Biblia ilisema wazi kwamba dunia ilikuwa mviringo au duara (Isaya 40:22). Watu wengine wa kale waliamini kwamba chini ya dunia alikuwepo jitu au tembo au kobe kubwa mno na kwamba alikuwa amebeba dunia mabegani mwake. Walakini, Biblia ilisema kwamba Mungu aliutundika ulimwengu pasipo kitu (Ayubu 26:7). Watu wa kale hawakujua jinsi ugonjwa unavyoenezwa. Mungu aliwapa watu wake sheria nyingi zilizoweza kuwakinga na maradhi. Ilikwa vigumu kwa watu wale kuelewa faida ya sheria hizo. Wakaona sheria nyingi kuwa ni upuzi tu. Lakini, watu ya sayansi siku hizi wametambua kwamba sheria hizo zilikuwa na hekima kweli kweli ya kukinga maradhi (Kutoka 15:26; Walawi 13:45,46; Kumbukumbu 23:12,13).

### 4. Mambo yaliyotabiriwa katika Biblia yaonyesha imetoka kwa Mungu.

Mwanadamu kwa nafsi yake hawezi kujua ni nini litakalotokea katika maisha yake hata kesho. Lakini, Biblia iliweza kueleza mambo mengi kabla hayajatokea. Kwa mifano: **1)** Katika Hosea 1:4,5,7 nabii alitabiri kwamba Mungu ataukomesha ufalme wa Israeli ila ufalme wa Yuda utaendelea. Mambo hayo yalitokea sawa sawa na utabiri wake. **2)** Katika Hosea 3:4,5 nabii alisema: *"Kwa maana wana wa Israeli watakaa siku nyingi bila mfalme, wala mtu mkuu, wala sadaka, wala nguzo, wala naivera, wala kinyago; baada ya hayo wana wa Israeli watarejea, na kumtafuta Bwana, Mungu wao, na Daudi, mfalme wao, nao watamwendea Bwana na wema wake kwa kicho siku za mwisho."* Mambo hayo nayo yalitokea yote. **3)** Katika Yoeli 2:28-32 nabii alitabiri mambo mbalimbali saba ambayo yote yalitimizwa siku ya Pentekoste ile ya Matendo mlango wa pili. **4)** Katika Yoeli 3:4-8 nabii alisema miji ya Tiro na Sidoni itapata mapigo makali. Ndivyo ilivyotokea. **5)** Katika Amosi 1:3-8 nabii alitabiri mambo kuhusu Dameski, Gaza, Ashdodi, na Ashkeloni ambayo yote yalitokea. **6)** Kitabu cha Obadia kinatabiri kwamba watu wa Edomu

wataangamizwa na wapagani na Wayahudi pia. Ndivyo ilivyotokea. **7)** Nahumu alitabiri kuangamizwa kwa Ninawi. Hayo nayo yalitokea. **8)** Kwa habari ya Yesu, manabii wa Agano la Kale walitabiri **mambo sitini** ambayo yote yalitimizwa katika maisha ya Yesu! Kwa mfano kitabu cha Isaya kiliandikwa mnamo **miaka 750 kabla ya kuzaliwa kwake Yesu**. Kitabu hiki kilitabiri mambo mengi sana kuhusu maisha na kifo cha Yesu ambayo yote yalitimizwa. Soma Isaya 53. Nabii Isaya asingalijua mambo hayo ikiwa Mungu asingalimwongoza! Hii ni mifano michache tu ya unabii wa Biblia uliotimizwa.

### 5. Tunaamini Biblia kwa sababu ya ushuhuda wa Wakristo wa kwanza.

Wakristo wasingalikubali kuteswa ikiwa wasingalijua uhakika wa mambo yale waliyokuwa wakiyahubiri. Maana, wengi walinyang'anywa mali zao, wengine walipigwa vibaya, wengine walifungwa gerezani, hata wengine wengi waliuawa kwa ajili ya ushuhuda wao. Walakini walikubali mambo hayo yote kwa sababu walimwona Yesu na kuthibitisha kwa macho yao kwamba alikufa na kufufuka tena! Je! wadhani watu wale wangekubali kufa kuyatetea mafundisho ya uongo?

### 6. Tunaamini kwamba Biblia ni kitabu cha Mungu kwa sababu maadui wa Biblia wameshindwa kuikomesha.

Watu wengi wamejaribu kuiharibu Biblia kwa njia ya kupinga mafundisho yake. Walakini, wameshindwa kwani Mungu ameilinda Biblia. **1)** Wengine walidai kwamba Biblia na mafundisho ya sayansi hayapatani. Lakini, kama tulivyoona tayari, Biblia ilieleza mambo mengi ya sayansi kabla wanadamu hawajakuwa na elimu ya kutosha kuyaelewa. Idadi kubwa ya wanasayansi wanaamini Mungu yupo na kwamba Biblia ni kitabu chake. Biblia haipingani na sayansi isipokuwa wapo watu wanaodai mambo fulani ya sayansi kuwa ni kweli ambayo hawawezi kabisa kuyathibitisha! **2)** Wengine walisema Biblia ni kitabu cha hadithi tu. Walidai kwamba mataifa kama Waedomu na Wamoabu hawakuwahi kuishi duniani hata ingawa Biblia inaeleza historia yao. Walakini, sasa wataalamu wamethibitisha kwamba mambo yote ya historia yaliyoandikwa katika Biblia ni kweli! **3)** Wengine wamesema kwamba mambo yale yaliyotabiriwa kuhusu Yesu yaliandikwa na Wakristo baada ya Yesu kuishi na kwamba Wakristo wanadanganya watu kusema yalitabiriwa kabla yake. Walakini vitabu vyote vinavyotabiri habari za Yesu vimo katika Agano la Kale ambalo Wayahudi wanasoma mpaka leo. Iwapo Wakristo wangalijaribu kubadili au kuongeza neno lo lote katika Agano la Kale, basi Wayahudi wangalikuwa wa kwanza kuwashitaki. Lakini, hata Wayahudi wasiomwamini Yesu wanaendelea kuvisoma vitabu vile vile kwa sababu wanajua vimetoka kwa Mungu. Isitoshe, zipo nakala za vitabu vile ambazo wataalamnu wamehakikisha kuwa ziliandikwa kabla ya kuzaliwa kwake Yesu. **4)** Maadui wengine wa Biblia wamejaribu kuiangamiza kabisa. (Soma habari ya mmoja wao katika Yeremia 36:1-4, 21-32 uone jinsi alivyoshindwa!) Warusi wamesema kwa muda mrefu kwamba hakuna Mungu. Isitoshe, wamejaribu kuvinyang'anya na kuviteketeza vitabu vyote vya Biblia katika nchi yao. Walakini, wameshindwa kabisa kabisa! Maana, sasa Warusi wamebadili siasa yao na karibu watu wote wanahamu kubwa kuisoma Biblia! Basi, jinsi Mungu alivyoilinda Biblia mpaka leo ni ishara kubwa kwamba imetoka kwa Mungu. Soma Isaya 40:8; Mathayo 24:35; na l Petro 1:23-25.

Kuna mambo mengine mengi yanayothibitisha kwamba Biblia imetoka kwa Mungu. Hatuna nafasi ya kuyataja mambo hayo yote, ila tutasoma baadhi ya mistari ya Biblia inayothibitisha ukweli huo.

Waandishi wa vitabu vya Biblia hawakuthubutu kusema kwamba maneno waliokuwa wakiandika yalikuwa maneno yao wenyewe. La! Bali twasoma:

"*. . . Unabii haukuletwa po pote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali* ***wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Miakatifu***." 2 Petro 1:21

Paulo alisema, *"Nayo* ***twayanena****, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho."* 1 Wakorintho 2:13

Mtume alisema, *"Kwa maana, ndugu zangu, injili hiyo niliyowahubiri, nawajulisha ya kuwa siyo ya namna ya kibinadamu. Kwa kuwa sikuipokea kwa mwanadamu wala* ***sikufundishwa na mwanadamu, bali kwa ufunuo wa Yesu Kristo.****"* Wagalatia 1:11-12

*"Kwa sababu hiyo sisi nasi twamshukuru Mungu bila kukoma, kwa kuwa, mlipopata lile neno la ujumbe la Mungu mlilolisikia kwetu, mlilipokea si kama neno la wanadamu, bali kama neno la Mungu; na ndiyo lilivyo kweli kweli; litendalo kazi pia ndani yenu ninyi mnaoamini."* 1 Wathesalonike 2:13

*"****Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu****, lafaa lawa* ***mafundisho****, na kwa* ***kuwaonya watu makosa yao****, na kwa* ***kuwaongoza****, na kwa* ***kuwaadibisha katika haki****; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."* 2 Timotheo 3:16-17

## TUSIONGEZE WALA TUSIPUNGUZE

Kwa sababu Biblia imetoka kwa Mungu, ni lazima kwa wanadamu kuiheshimu na kuifuata bila kuongeza wala kupunguza neno. Mahali pengi katika Biblia tunaonywa kutokupita maneno ya Mungu.

*"Usiongeze neno katika maneno yake; Asije akakulaumu, ukaonekana u mwongo."* Mithali 30:6

*"Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine; lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi* ***au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe****."* Wagalatia 1:6-8

*"Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabi wa kitabu hiki,* ***Mtu ye yote akiyaongeza, Mungu atamwongeza hayo mapigo*** *yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atanwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zineandikwa katika kitabu hiki."* Ufunuo 22: 18-19

*"Yesu alisema, "Mbingu na nchi zitapita; lakini* ***maneno yangu hayatapita kamwe****."* Mathayo 24:35

*"Yeye anikataaye mimi, asiyeyakubali maneno yangu, anaye amhukumuye:* ***neno hilo nililolinena ndilo litakalomhukumu siku ya mwisho****."* Yohana 12:48

*"Kila apitaye cheo, wala* ***asidunu katika mafiundisho ya Kristo, yeye hana Mungu****. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia."* 2 Yohana 1:9

*"Akajibu, akawaambia,* ***Mbona ninyi nanyi huihalifu amri ya Mungu kwa ajili ya mapokeo yenu****? . . . Watu hawa huniheshimu kwa midomo; Ila mioyo yao iko mbali nami. Nao* ***waniabudu bure, Wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu****…Waacheni; hao ni viongozi vipofu wa vipofu. Na kipofu akimwongoza kipofu mwenzake, watatumbukia shimoni wote wawili."* Mathayo 15:3,8-9,14

Baadhi ya watu hudhani kwamba watu wote wanaomwamini Yesu wataokoka hata ingawa hawafuati amri zake zote. Walakini, Yesu ametuonya:

*"Ingieni kwa kupitia mlango ulio mwembamba; maana mlango ni mpana, na njia ni pana iendayo upotevuni, nao ni wengi waingiao kwa mlango huo. Bali mlango ni mwembamba, na* ***njia imesonga iendayo uzimani, nao waionao ni wachache. . . Si kila mtu aniambiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba*** *yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwajina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe; ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu."* Mathayo 7: 13-14,21-23

***************************************************************************************

Baada ya kuyajibu maswali yote uandike jina lako na anwani yako na utume karatasi ya maswali kwa anwani iliyoandikwa hapa chini. Baada ya kuisahihisha tutairudisha kwako pamoja na somo jipya.

***KANISA la KRISTO***

***Tanzania***

### *MASWALI*

1. Neno Biblia maana yake nini? ________________
2. Katika Biblia vimo vitabu vingapi? ________________
3. Katika sehemu ya Biblia iitwayo Agano la Kale vimo vitabu vingapi? ________________
4. Vitabu vya Biblia viliandikwa na watu wangapi? ________________
5. Kuandikwa kwa vitabu kulichukua muda wa miaka mingapi? ________________
6. Je! Waandishi wa vitabu hivi walijuana na kushauriana katika kuandika kwao?________________
7. Nabii Isaya alitabiri kifo cha Yesu miaka mingapi kabla hajazaliwa Yesu? ________________
8. Katika kuandika Biblia wanadamu walikuwa wakiandika maneno yaliyotoka kwa nani? (2 Petro 1:21) ________________
9. Nani aliwaongoza katika kuandika maneno ya Mungu? (2 Petro 1:21) ________________
10. Mambo yale yaliyohubiriwa na Paulo yalitoka kwa nani? (1 Wakorintho 2:13) ________________
11. Je! Yalikuwa mafundisho yaliyotungwa na wanadamu? (Wagalatia 1:11-12) ________________
12. Wakristo walitambua kwamba maneno yale yaliyohubiriwa na Paulo yalikuwa maneno ya nani? (1 Wathesalonike 2:13) ________________
13. Maandiko yaliyotoka kwa Mungu yafaa kwa mambo manne. Uyataje hapo penye mistari ifuatayo: (2 Timotheo 3:16-17) ________________
14. Kwa kuwa Biblia inatukamilisha, je! Tunahitaji vitabu vingine vya mapokeo ya wanadamu kama katekisimu, misale, au liturgia? (2 Timotheo: 3:16-17) ________________
15. Mtu akiongeza neno katika maneno ya Mungu ataonekana kuwa nani? (Mithali 30:6) ________________
16. Je! Watu wale wanaobadili injili ya Kristo wanatusaidia au wanatutaabisha? (Wagalatia 1:6-8) ________________
17. Mwisho wake mtu yule ambaye anabadili maneno yale yaliyohubiriwa na mitume utakuwaje? (Wagalatia 1:6-8) ________________
18. Je! Malaika wanaruhusiwa kubadili maneno yaliyoandikwa katika Biblia? (Wagalatia 1:6-8) ________________
19. Mtu ye yote akiongeza lo lote katika kitabu cha Mungu atapata nini? (Ufunuo 22:18-19) ________________
20. Je! Maneno ya Yesu yatapita? (Mathayo 24:35) ________________
21. Siku ya mwisho tutahukumiwa kwa maneno ya nani? (Yohana 12:48) ________________
22. Je! Viongozi wa dini wanaobadili mafundisho ya Yesu hawana nini? (2 Yohana 1:9) ________________
23. Yesu alisema kwamba watu walikuwa wakihalifu amri za Mungu kwa ajili ya nini? (Mathayo 15:3) ________________
24. Tunamwabudu Mungu bure tunapofundisha mafundisho yaliyo maagizo ya nani? (Mathayo 15:8-9) ________________
25. Aliye kipofu katika dini akimwongoza kipofu mwenzake, nani atatumbukia shimoni? (Mathayo 15:14) ________________

*************************************************************************************

Baada ya kuyajibu maswali yote uandike jina lako na anwani yako na utume karatasi ya maswali kwa anwani iliyoandikwa hapa chini. Baada ya kuisahihisha tutairudisha kwako pamoja na somo jipya.

Jina lako ………………………………………………

Anwani yako …………………………………………

***KANISA la KRISTO***
***Tanzania***